

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

Anwani ya simu: UCHUNGUZI  
Simu Nambari: +2550262782777  
Fax Na: +255 026 2782777  
Unapojibu tafadhali taja:



TAKUKURU (M),  
MTAA WA KWIVAHA,  
S. L. P 629,  
59101NJOMBE.

TAREHE: 12/11/2018

## TAARIFA KWA UMMA

### TAARIFA YA UTENDAJI KAZI TAKUKURU MKOA WA NJOMBE KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBER 2018

TAKUKURU Mkoa wa Njombe imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa (PCCA NA.11/2007). Katika kipindi tajwa hapo juu TAKUKURU (M) Njombe imeweza kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo.

#### 1. UCHUNGUZI NA MASHTAKA

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2018, jumla ya taarifa za vitendo vya rushwa 94 zilipokelewa katika vituo vyetu vya Njombe, Makambako, Makete na Ludewa na kufanyiwa kazi kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

Katika kipindi hiki jumla ya kesi 5 zilifunguliwa mahakamani na 1 kati ya hizo ilishinda na zingine bado zinaendelea mahakamani.

KITUO	Taarifa zilizopokelewa	Majalada yaliyokamilika			Majalada yaliyopelewa HQ			Kesi zilizofunguliwa		
		L	U	%	L	U	%	L	U	%
NJOMBE	33	3	4	100	3	6	100	3	3	100
MAKAMBAKO	7	2	3	100	2	0	0	0	0	0
MAKETE	25	2	3	100	2	4	100	2	0	0
LUDEWA	29	2	1	50	2	1	50	2	2	100
JUMLA	95	9	10	87.5	9	11	62.5	9	5	50

Kesi zilizofikishwa mahakamani katika kipindi hiki ni pamoja na mabaraza ya kata na watendaji wa kata na vijiji kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa na kushindwa kutoa huduma na haki kwa wananchi hususan katika maeneo ya vijijini. Takwimu zinzonyesha kuwa utendaji kazi wa TAKUKURU (M) Njombe umefikia malengo kwa mujibu wa mpango mkakati wa TAKUKURU.

## 2. ELIMU KWA UMMA

Katika kipindi cha robo mwaka yaani Julai - Septemba 2018, TAKUKURU Njombe imetekeleza majukumu ya kuhamasisha na kuelimisha umma na wadau mbalimbali ili waweze kushiriki mapambano dhidi ya rushwa. Vigezo na matokeo ya uelimishaji katika robo ya kwanza ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

KITUO	Kufungua Klabu			Kuimarisha klabu			Mijadala ya wazi			Semina			Vipindi			Maonesho		
	L	U	%	L	U	%	L	U	%	L	U	%	L	U	%	L	U	%
NJOMBE	8	3	37.5	14	1	7.1	6	17	100	3	11	100	2	2	100	2	2	100
MAKETE	8	0	0	14	39	100	6	1	16	3	10	100				2	2	100
LUDEWA	8	0	0	14	6	42	14	6	42	3	0	0				2	0	0
MAKAMBAKO	3	2	67	3	2	67	3	7	100	3	0	0						

## 3. UCHAMBUZI WA MIFUMO

Katika kipindi cha July na September 2018, TAKUKURU (M) Njombe imeweza kufanya uchambuzi wa mifumo kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:

N A	OFISI	UCHAMBUZI WA MIFUMO			WARSHA			UFUATILIAJI		
		L	U	%	L	U	%	L	U	%
1	NJOMBE	2	2	100	1	1	100	1	0	0
2	MAKETE	1	1	100	1	1	100	1	0	0
3	LUDEWA	1	1	100	1	0	0	1	0	0
4	MAKAMBAKO	1	2	100	1	2	100	1	0	0

#### **4. UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO**

Katika kipindi cha Julai -Septemba 2018 TAKUKURU (M) Njombe imeweza kufuatilia na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kuhakiki ubora na thamani ya pesa za umma. Aidha ufuatiliaji huu ulijikita katika miradi mbalimbali iliyoainishwa na kutolewa kasoro na baadae kukataliwa na wakimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka 2018. Baadhi ya miradi iliyofuatiliwa ni kama ifuatavyo.

- (A) Mradi wa Maji kijiji cha ukalawa wenye thamani ya Tshs 562,852,061.86. Baada ya ufuatiliaji wa awali TAKUKURU ilibaini mapungufu makubwa katika mradi huu na kuamua kufungua jalada la uchunguzi. Uchunguzi wa tuhuma bado unaendelea na matokeo yake yatatangazwa kwa umma.
- (B) Ujenzi wa zahanati ya kidegembe katika halmashari ya wilaya ya Njombe wa thamani ya Tshs 60,430,800/baada ya ufuatiliaji wa awali TAKUKURU iliweza kubaini kuwa mradi huu ulikidhi vigezo na thamani ya pesa ila kulikuwa na mapungufu katika kutoa taarifa iliyowasilishwa kwa wakimbiza mwenge wa uhuru.
- (C) Mradi wa vibanda Njombe mji (pombe shop). Mradi huu unathamani yaa Tshs 399,980,816.00/ na ulitekelezwa na halmashauri ya mji Njombe. Baada ya ufuatiliaji ilibainika kuwa pamoja na taarifa kukosewa bado mradi ulikuwa na mapungufu mbalimbali ambapo baada ya kufuatilia yalirekebishwa na mradi ulifunguliwa na sasa unatumika.
- (D) Mradi wa ujenzi wa madarasa mawili kwa ufadhili wa TASAF katika kijiji cha Madobole Njombe. Mradi huu ulikuwa na thamani yaa Tshs . Baada ya Tshs 63,848,007.00/ baada ya ufuatiliaji TAKUKURU imebanini mapungufu mengi ikiwa ni pamoja na dalili za kuwepo ubadhilifu na hivyo kuanzisha jalada la uchunguzi kubaini ukweli na taarifa itatolewa baadae.
- (E) Mradi wa unuuzi wa pikipiki za watendaji wa kata katika halmashari ya mji Njombe wenye thamani ya Tshs 9200, 000/. Baada ya ufuatiliaji wa awali makosa ya usajili yalirekebishwa na pikipiki kukabidhiwa kwa watendaji husika.

## **5. WITO**

TAKUKURU(M) Njombe tunatoa wito kuwa wadau na wananchi wa mkoa wa Njombe kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU kwa kutoa taarifa na kukemea vitendo vya rushwa katika mkoa wetu wa Njombe na vitongoji vyake na sisi tutachukua hatua stahiki.

Imetolewa na  
**CHARLES NAKEMBETWA SHAMSULLA**  
**MKUU WA TAKUKURU [M]**  
**NJOMBE**  
**14.11.2018**